JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA NNE

**04 NOVEMBA, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA NNE – TAREHE 04 NOVEMBA, 2016

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**41. MHESHIMIWA SIXTUS RAPHAEL MAPUNDA (MBINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Mbinga inatoa huduma kwa Halmashauri nne yaani Mbinga Mjini, Mbinga Vijijini, Nyasa na baadhi ya Kata za Songea Vijijini hali inayopelekea Hospitali hiyo kuwa na upungufu wa vitendeakazi, wodi na vyumba vya kulaza wagonjwa, chumba cha upasuaji, gari la kubebea wagonjwa pamoja na ukosefu wa Madaktari Bingwa:-

Je, ni lini Serikali itaboresha Hospitali hiyo ili iweze kutoa huduma inayotarajiwa.

**42. MHESHIMIWA AMINA SALEH MOLLEL (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Sera ya Elimu inasema mlinganyo wa vyoo kwa wanafunzi wa kike uwe choo kimoja kwa wasichana 20 na choo kimoja kwa wavulana 25:-

Je, utekelezaji wa Sera hiyo kwenye eneo hili ukoje.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**43. MHESHIMIWA ELIAS JOHN KWANDIKWA (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini Serikali itatambua mchango mzuri wa Wasimamizi wa Rasilimali Fedha, Wahasibu Viongozi (*Chief Accountants*) walioko kwenye Wizara na Idara za Serikali kwa kuwapandisha kwenye ngazi za Ukurugenzi ili waweze kuleta tija zaidi kwa ushiriki wao katika maamuzi ya Menejimenti ya Wizara/Idara zao.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**44. MHESHIMIWA STANSLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):- Kutokana na athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea hivi sasa Duniani pamoja na uharibifu mkubwa wa mazingira Mkoa wa Simiyu ni moja kati ya maeneo yaliyoathirika kwa kiwango kikubwa na kuna uwezekano mkubwa wa Mkoa huo kugeuka kuwa jangwa:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuunusuru Mkoa huo na hali hiyo;

(b) Kwa kuwa hali hiyo inaathiri shughuli za kilimo hasa cha umwagiliaji; Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mazingira ya Mito na Mabwawa yanatunzwa.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**45. MHESHIMIWA FAIDA MOHAMMED BAKAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Matumizi ya dola katika maeneo mengi

nchini ndiyo sababu kubwa ya kushuka kwa thamani ya fedha yetu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha matumizi ya fedha yetu kwa Wananchi wake pamoja na wageni nchini ili kukuza thamani ya fedha yetu na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

**46. MHESHIMIWA KABWE RUYAGWA ZITTO (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa Maji wa Manispaa ya Kigoma Ujiji unaogharimu shilingi bilioni 32 ambao unafadhiliwa na Shirika la KFW la Ujerumani na Jumuiya ya Ulaya ulipangwa kukamilika Mwezi Machi, 2015:-

(a) Je, kwa nini mradi huo umechelewa kukamilika kwa mujibu wa Mkataba;

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya Mkandarasi kwa kuchelewa kukamilisha mradi huo.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**47. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) kupitia mtandao wa *Twitter* na Vyombo vya Habari alitangaza kuzuia Timu yoyote katika kundi C la Ligi Daraja la Kwanza kupanda daraja kabla ya mechi zao kukamilika na kabla ya vikao halali vya uchunguzi kufanyika:-

Je, Serikali haioni kwamba maamuzi yalifanywa kinadharia na uonevu mkubwa kwa timu ya Geita Gold Sport Club.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

**48. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIAH BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi:- Ni Sera ya Taifa kuwa katika kila Wilaya kuwe na Chuo cha Ufundi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha Ufundi katika Wilaya ya Geita.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 49. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Msitu wa Shagayu ndio wenye vyanzo vingi vya Mito katika Jimbo la Mlalo; Msitu huu uliungua takribani hekari 49 mwaka 2012:-

Je, ni lini Serikali itapanda miti katika eneo lililoungua ili kulinda vyanzo vya maji.

### 50. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Serikali ilielekeza nguvu zake katika kutangaza vivutio vya Utalii na wawekezaji kuja Kanda ya Kusini ili kupunguza msongamano wa utalii Kaskazini mwa Tanzania:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani Serikali imeyatangaza maporomoko ya Kalambo ambayo ni ya pili Afrika baada ya yale ya Victoria kuwa kivutio cha Utalii;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Hifadhi ya Msitu wa Kalambo pamoja na maporomoko haya yanakuwa chini yake kupitia Shirika lake la TANAPA.

## WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

**51. MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL (BABATI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni kwa nini Serikali imekuwa hairudishi katika Halmashauri zetu 30% ya mauzo ya viwanja.

**52. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Wananchi waliojenga nyumba katika maeneo ambayo hayajapimwa wanapopata kesi hasa kwenye Mahakama ya Wilaya wanatakiwa kutoa Hati au Ofa lakini kwa kukosa nyaraka hizo ndugu au jamaa wanakosa kudhaminiwa:-

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kupandishia thamani ya makazi ya Wananchi hao.

53. **MHESHIMIWA DEVOTHA MATHEW MINJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kupunguza gharama za upimaji viwanja ambazo ni kubwa sana ili kumwezesha kila Mtanzania kupata huduma hiyo na kuondoa migogoro ya ardhi.

## III. KAULI ZA MAWAZIRI:

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa Mwaka 2016 *(The Media Services Bill, 2016).*

**DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH**
**04 NOVEMBA, 2016** | **KATIBU WA BUNGE**